**_TALKING NOTES ZA MHE._ THOBIAS ANDENGENYE WAKATI UZINDUZI WA MNARA WA TTCL WILAYA YA BUHIGWE NA MAENEO JIRANI WILAYANI BUHIGWE**

**14 DISEMBA, 2021.**

**==================================**

**UTANGULIZI**

Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango- Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji- Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

Mhe. Dkt. Zainab Chaula- Katibu Mkuu- Wazara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Ndg. Waziri Kindamba -Mkurugenzi Mtendaji wa TTCL

Ndg. Richard Malulu Mayongela- Mjumbe wa Bodi ya TCCL

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Mhe. Makamu wa Rais**

**Naomba niwatambulishe kwako**

Ndg. Amandus Nzamba –Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa

Rashid Kassim Mchatta-Katibu Tawla wa Mkoa

Kamati ya Ulinzi ya Mkoa,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya

Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kigoma Mliopo.

Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Viongozi wa Dini

Viongozi wa Vyama vya Siasa

Wananchi wote waliopo katika tukio hili

Waandishi wa Habari

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya ya kuweza kujumuika hapa leo. Nikushuru wewe Mhe. Maku wa Rais kwa kuja kutuzindulia mnara huu wa mawasiliano katika Wilaya ya Buhigwe na maeneo jirani. Shukrani zangu za dhati kwa Shirika la Mawasiliano Tanzania TTCL kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa hatua ya kuboresha Mawasiliano hapa Wilaya ya Buhigwe na maeneo jirani. Aidha; napenda niwakaribishe wageni wotee wanaotoka nje ya Mkoa huu **KARIBUNI SANA.**

**Mhe. Makamu wa Rais**

Mkoa wa Kigoma upo shwari, wananchi wanaendele na shughuli za maendeleo za kila siku.

Kwa upande wa shughuli za Serikali tunaendele kusimamia shughuli za maendeleo. Mkoa ulipokea zaidi ya Bilioni 15 kutoka mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya uviko-19. Shughuli za usimamizi wa miradi mbalimbali ya maendelo zinaendeleo ikiwemo ukamilishaji wa miundombinu ya madarasa 638 (ambapo Vyumbna vya madarasa 86 katika shule shikizi, madarasa 550 shule za sekondari na mabweni 02 katika shule za Watoto wenye mahitaji maalum).

**Mhe. Makamu wa Rais**

Aidha, Mkoa wa Kigoma umepokea fedha nje ya bajeti yake Zaidi ya Bilion 19 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Tunaomba utufikishie shukrani zetu za dhati kwa Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jmhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nia yake ya dhati ya tuletea fedha za maendeleo na kuendelea kuufungua Mkoa wetu wa Kigoma.

**Mhe. Makamu wa Rais**

Kwa tukio hili la leo napenda kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma kuishukuru Serikali kwa kuondoa changamoto ya muda mrefu ya mawasiliano ya simu katika Wilaya ya Buhigwe na maeneo jirani.

Mkoa wa Kigoma umekuwa nachangamoto ya Mawasiliano hususan katika Wilaya na maeneo yaliyopo pembezoni yaani yanayopakana na nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Hata hivyo kumekuwepo na juhudi za makusi zinazofanywa na serikali ya awamu ya Sita kukabiliana na changmoto ya mawasiliaano mkoani kigoma mathalani, katika Wilaya ya Kasulu Shirika la Utangazaji Tanzania TBC limepatiwa eneo la kujenga Mnara katika halmashauri ya kasulu mji. Aidha katika Wilaya ya uvinza Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umepatiwa eneo kwa ajili ya kujenga mnara wa mawasiliano; juhudi hizi zinalenga kuimarisha utoaji huduma za mawasiliano nchini ili kuhakikisha ufikiaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo yote yenye mawasiliano hafifu pamoja na yale yasiyo na huduma hiyo kabisa.

**Mhe. Makamu wa Rais**

Mkoa wa Kigoma una vituo vya redio Sita (6) (sita), Redio Joy, Uvinza FM, Redio Kwizera, Kikaora FM ambazo usikivu wake ni kwenye baadhi ya maeneo tu.

Ukiwa kwenye mwambao wa ziwa Tanganyika upande wa Kusini (Wilaya ya Uvinza) mara nyingi redio kutoka DR Congo zinatoa usikivu zaidi, na mwambao wa ziwa upande wa Kaskazini. Wilaya za Buhigwe, Kasulu, Kibondo na Kakonko usikivu wa Redio unatoka Burundi. Kwa ujumla sikivu wa Redio zetu za ndani ni hafifu na mara nyingi maeneo ya pembezoni zinasikika redio za nchi jirani. Kwenye upande wa Televisheni wananchi wanapata chaneli nyingi za Kitaifa na Kimataifa.

**Mhe. Makamu wa Rais**

Ni imani yetu wana Buhigwe na Kigoma nzima mnara huu utakuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo mbali na mawasiliano mawasiliano haya utakuza ajira katika maeneo ambayo tunaishi, sambamba na kuchangamkia fursa ambazo zinatokana na uwepo wa Mtandao huu. Fursa hizo pamoja na Kusajili laini, fursa ya kuwa wakala wa kuuza VOCHA na uwakala wa T.PESA. Uwepo huduma ya mawasiliano itaondoa changamoto iliyokuwa inawakuta wakazi maeneo haya wa kukosa huduma ya mawasiliano ya simu kwa muda mrefu, hivyo mawasiliano ya simu yataleta tija kwa wananchi sambamba na kufungua milango ya fursa ya ajira na kujiongezea kipato.

Uwepo wa mnara huu utawezesheza uwepo wa mtandao wa uhakika utakaowawezesha sasa kutumia uwepo wa mawasiliano ya simu katika kutafuta fursa za maendeleo, ikiwa pamoja na kutafuta masoko ya mazao yao.

Sasa wananchi wa Buhigwe na  watapata huduma ya kupiga simu, , intaneti na huduma ya miamala ya kifedha kutuma, kupokea na kutoa pesa, kununua muda wa maongezi, huduma za kibenki, kununua umeme, ving'amuzi kwa urahisi zaidi.

Kwa dhati kabisa naipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kuhakikisha inapeleka huduma za mawasiliano ya simu maeneo ambayo bado yana changamoto ya mawasiliano hasa maeneo ya vijijini na pembezoni mwa mipaka ya nchi yetu kama Mkoa wa Kigoma. Niwashukuru pia Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) katika adhima ya kufikisha mawasiliano vijijini.

**Mhe. Makamu wa Rais**

Kwa niaba ya Wananchi wa Buhigwe tunaahidi kuitunza na kuilinda miundombinu miundombinu ya mnara huu na miundombinu ya mingine mawasiliano ya Shirika la Mawasiliano Tanzania.

Baada ya kusema hayo naomba kuwakaribisheni nyote katika Mkoa wa Kigoma hususan kwenye shughuli hii muhimu kwa maendeleo ya wnanchi wa Mkoa wa Kigoma.

**Mhe. Makamu wa Rais nakushukuru sana kunipatia fursa hii.**

**====================================================**